

Jina.....Nambari yako.....
Shule.....
Tarehe.....Sahihi ya Mtahiniwa.....

102/2

KISWAHILI

Karatasi ya 2

Kidato cha 4

LUGHA Ufahamu, Muhtasari,

Matumizi ya lugha na Isimu jamii)

April 2013

Muda: Saa $2\frac{1}{2}$

MTIHANI WA PAMOJA WA PENTAGON - 2013

WILAYA YA WARENG

Kiswahili

Karatasi ya 2

MAAGIZO

- Andika jina lako na namba yako katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Tia sahihi yako na tarehe ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu.
- Jibu maswali yote. Andika majibu yako katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu hiki cha maswali.

MATUMIZI YA MTAHINI

Swali	Upeo	Alama
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
JUMLA	80	

1. UFAHAMU (alama 15)

Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Kila magharibi tunafanya shughuli fulami tena na tena; tunakuwa na hakika kuwa tutapata chajio na wanetu wataakaa kufanya kazi zao za ziada za shule. Wakati mwengine wakipata swali gumu watakimbia ukumbini tunapoipumzisha, tukijaribu kupumzika baada ya kazi ngumua kuuliza, "mama jina la kifunguo cha mlango huitwaje kwa Kiswahili?" Kadiri ninavyokumbuka kutoka mafunzo yangu, ni sharti nikubali kuwa silihui jibu lake. Sikumbuki ikiwa niliwahi kusoma majina ya sehemu mbalimbali za mlango shulenii, au ikiwa nilikuwa shule siku hiyo. Kwa hivyo tulikulia katika mfumo wa elimu usiokuwa na matakwa mengi, ninawahurumia wanetu siku hizi wanavyokwenda shule na mabegi mabegani.

Katika shule nyingi watoto hasa wa madarasa ya mtihani, wanatarajiwa kuwa darasani saa moja asubuhi na kubakia baada ya shule kifungwa ili kupata mafunzo ya ziada. Katika shule nyingine, watoto wanatarajiwa shulenii wikendi ili kukamilisha silabasi. Mfumo wetu wa elimu umeshutumiwa kuwanyima wanafunzi utoto wao ukisisitiza kupasi mtihani ~~na masomo~~ chungu nzima. Kwa muda mrefu kumekuwa na jaribio la kufikiria tena kuhusu mfumo wa elimu 8-4-4. Lakini watoto bado wanabebe mzigo mzito wa mfumo ambaa huruhusu muda mchache wa kucheza.

Watahiniwa wa mtihani wa kidato cha nne na wazazi wao walingojea kwa ghamu kutangazwa matokeo ya mwaka jana na wizara ya elimu. Matokeo ambayo yatakuwa kigezo cha watakaokwenda vyuo vikuu vya umma na kupata digrii.

Inavyotarajiwa, kulikuwa na shangwe katika viambo vingi vya wanafunzi waliofuzu, picha zao zilivyotokea magazetini na wakawa nyota wa siku hiyo. Ni muhimu kusherehekeea bidii za wanetu, tuisihau mfumo unaowatayarisha vyema kwa mtihani haufanyi hivyo kuwatayarisha kukabiliana na maisha. Kweli, nahusudu hitimu za akademia lakini ukweli sharti usemwe, kuna elimu ninayoiensi mno. Ni elimu inayopatikana katika mafunzo ya tajriba na kufunzwa na 'walimu' wasiowerevu. Shulenii, watakwambia elimu ni ufunguo unaofungua milango yote lakini hawatakufunza jinsi ya kukabiliana na watu. Hawakufunzi kuwa watu watasihau aghalabu ulichosema au kutenda, lakini hawatasihau ulivyofanya wahisi. Watakufunza kusoma vitabu shulenii lakini hawatawahi kukufunza jinsi ya kusoma uso, au kuchambua kindani, ukichunguza maswala yote yaliyofichika. Watu watakufunza kusadiki ukweli lakini tajriba itakufunza kuamini ukakamavu wako. Shulenii watakufunza fomula za hisabati lakini watakosa kukuhimiza jinsi ya kutambua fursa na kuinyakua. Hawatakufunza umuhimu wa kusubiri.

Watakufundisha kutengeneza mbinu ya kibiashara lakini si sayansi inayowafanya walioacha shule kupata mamilioni kutumia wazo la mtu mwengine. Labda mpumbavu aliyeelimika sana atakwambia ukianguka mtihani, umejiingiza katika maisha ya utaka. Mafunzo ya maisha yatakufunza sharti utafute shabaha na nafasi ili upate ujira. Shulenii watoto werevu ndio wanaopendwa. Katika maisha ni wale wanaojua kuishi na wengine. Shule itakujaza na maelezo lakini haitakupa uwajibikaji na **maadili**. Itafundisha watoto historia subira, au haitawafanya kukubali mawazo au tamaduni tofauti. Watoto watajifunza jiografia ya dunia lakini si nafasi yao duniani. Watajifunza lugha lakini si aghalabu jinsi ya kuwasiliana vyema.

Shule inaweza kuwasaidia watoto kupata elimu ambayo sharti, inatumainiwa kuwapa zaidi yajaribio katika maisha. Lakini wazazi walezi na wengine wanaowazunguka ndio watawafundisha **stadi** watakazohitajia kuendelea kuishi katika ulimwengu halisi.

Maswali

- (a) Kwa mujibu wa taarifa hii, watu wana kaida zipi? (alama 2)

- (b) Thibitisha kuwa “watoto si watoto tena” ukirejelea taarifa. (alama 4)

- (c) Kwa kutumia mifano eleza aina za elimu zilizojadiliwa katika taarifa. (alama 2)

- (d) Eleza ulemavu wa mfumo wa elimu wa 8: 4: 4. (alama 4)

- (e) Toa suluhisho la tatizo la upungufu wa mfumo wa elimu. (alama 1)

- (f) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa. (alama 2)

i) maadili _____

ii) stadi _____

2. MUHTASARI (alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuatia.

Katika miaka ya hivi karibuni, maduka ya kuuza dawa za matibabu kwa binadamu na mifugo yameongezeka kwa kiwango kikubwa sana. Wafanya biashara wengi bila kuzingatia kanuni za taaluma za dawa na matibabu.

Wameingilia biashara hii ya kuuza dawa kiholela, wakishinikizwa na tamaa ya kupata pesa za haraka. Mathalani, ukitembea katika mitaa mijini na vijijini utapata maduka yanayouza dawa yamepangana kando ya njia na vijia na kupambwa kwa ajili ya kuwavutia wateja haraka.

Hakuna ubaya wowote kwa mtu ye yeyote kufanya biashara yoyote, hasa ikieleweka kuwa ni njia mojawapo ya kuinua uchumi wa nchi yetu na kuifanaya kufikia kilele cha maendeleo makubwa. Hata hivyo, ni bora kila shughuli ya biashara ifanywe kwa njia isiyohatarisha maisha ya binadamu. Hii ni kwa sababu ukiwachunguza vyema wengi wa wahudumu wanaouza dawa kaika maduka haya, utagundua kuwa hawajahitimu katika taaluma za dawa na matibabu.

Ni jambo lisilopingika kuwa biashara ya dawa za matibabu inahitaji utaalamu wa hali ya juu na kwa hivyo haiwezi ikaendeshwa na wanagenzi na makurutu. Ni lazima, kwa hivyo wenye biashara za aina hii kuwaajiri wahudumu wenye elimu na ujuzi katika mambo ya dawa. Serikali inao wajibu wa kuchukua hatua kabambe kuhakikisha kuwa

wanaoanzisha na kuhudumu katika biashara za kuuza dawa wanaelewa na wana elimu ya kutosha katika madawa. Hii itasaidia kukabiliana na matumizi mabaya ya dawa za matibabu.

Inafahamika ya kwamba dawa ni sumu na iwapo mgonjwa atapewa dawa isiyofaa bila shaka ataathirika kiafya kutokana na sumu ilio ndani ya dawa hiyo. Aidha katika kipindi cha miaka kumi hivi iliyopita kumekuwa na visa vya baadhi ya dawa za matibabu kukosa kufanya kazi kutokana na kutumiwa vibaya. Mfano mmoja ni dawa aina ya "Chloroquin" iliyotumika katika kutibu ugonjwa wa Malaria kwa muda mrefu kwa kiwango kikubwa cha mafanikio ambayo sasa hautumiki tena kwa ajili ya viini kuwa sugu. Huu usugu ultokana na matumizi mabaya yaliyochangiwa na baadhi ya wafanyibiashara wa dawa za matibabu wasiohitimu.

Wahenga walinena kuwa ni bora kuzuia kuliko kuponya. Ni vyema ikiwa serikali itaacha kujikokota katika swala hili muhimu na kuwakomesha wanaohatarisha maisha na afya ya wananchi wake. Vilevile wizara ya afya inafaa iwe ikifanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye maduka yote ya dawa na kuwafurusha wanagenzi wasio na elimu kuhusu dawa wanazouza kwa wateja. Wananchi nao wnafaa watahadhari wanapoenda madukani kununua dawa kwani kuna baadhi ya wauzaji wasiolewa chochote madhali aso hadhari ni ng'ombe.

(Utatuzwa hadi alama 2 za utiririko kijumla)

Maswali

- (a) Fupisha aya mbili za kwanza. (maneno 45 - 55) (alama 5)

Nakala chafu

Jibu

- (b) Eleza mambo yote muhimu yanayozungumziwa katika aya tatu za mwisho. (maneno 60 - 70) (alama 8)

Matayarisho

Jibu

3. **MATUMIZI YA LUGHA** (alama 40)

(a) Eleza tofauti mbili za sauti hizi: /f/ na /d/ (alama 2)

(b) Tambua aina za viambishi katika neno ‘walao’ (alama 2)

(c) Yakinisha sentensi ifuatayo. (alama 2)
Mwandishi asingeenda Luanda asingepata habari

(d) Changanua sentensi hii kwa njia ya jedwali. (alama 4)
Walimu wanafundisha na wanafunzi wanasikiliza kwa makini.

- (e) Bainisha matumizi ya -ki- - katika sentensi ifuatayo; (alama 2)
Kijibwa hiki kitazama kikiingia mtoni.
-

- (f) Unda nomino moja moja kutokana na vitenzi hivi: (alama 1)
i) nyoa
-

- ii) kulea
-

- (g) Tunga sentensi kwa kutumia kitenzi ‘oa’ kwa kuzingatia kauli ya kutendwa. (alama 2)
-

- (h) Tambua kihusishi na kisha ueleze ni cha aina gani katika sentensi hii. (alama 2)
Shule hii ni bora kuliko ile nyingine.
-

- (i) Bainisha maana mbili za neno ‘kijusi’ kwa kutungia sentensi mbili. (alama 2)
-

- (j) Eleza maana tatu zinazojitokeza katika sentensi. (alama 3)
Kamau amenunua kitabu chake.
-
-

- (k) Tambua aina za shamirisho kwenye sentensi;
Cheptoo alifyeka nyasi kwa panga (alama 2)
-

- (l) Andika katika usemi wa taarifa. (alama 3)
Askari : Nitawaonyesha nikiwaona
-

- (m) Weka katika kinyume: (alama 2)
Mwalimu alitawanya karatasi ofisini.
-

- (n) Andika kwa hali timilifu. (alama 1)
Kisorio atafaulu na kwenda chuongi
-

- (o) Andika katika ukubwa. (alama 2)
Mwizi aliiba kikapu na ng’ombe
-

- (p) Weka nomino hizi katika ngeli zake: (alama 1)
i) Mvua
-

ii) Nokoa

(q) Andika kwa wingi
Iwapo utafika mapema utamwona. (alama 2)

(r) Nyambua kitenzi ‘ja’ katikahali ya: (alama 2)

i) Kutendeshea

ii) Kutendeshwa

(s) Tumia alama hii ya uakifishaji katika sentensi. (alama 1)
Vifungo

Eleza;

i) Maana ya kitawe (alama 1)

ii) Toa mfano mmoja wa kitawe na udhihirishe. (alama 1)

4. **ISIMUJAMII** (alama 10)

(a) Eleza manufaa matano yanayopatikana kwa kutumia Kiswahili bungeni. (alama 5)

(b) Lughu katika muktadha wa bunge huzingatia mambo gani? (alama 5)

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com